

**Swahili transcript:**

Katika suala zima la muziki Tanzania ni kwamba katika miaka ya hivi karibuni aah!kumekuwa na mwamko mkubwa sana wa muziki wa injili. Tanzania tuna muziki wa aina mbalimbali,kuna muziki wa dansi, kuna muziki huu wa kizazi kipya (bongo flava) ni muziki ambao unajulikana wa kundi hili la vijana ambao wanaibukia katika muziki, kwa hiyo ni tunaita muziki wa kizazi kipya. Pia vilevile kuna muziki wa jadi, na kuna huu muziki wa nyimbo za injili. Na katika miaka ya hivi karibuni ni kwamba muziki wa injili unaonekana wenyewe kuwa ndio kumepanda chati, yaani ni kwamba umekuja juu na unaididimiza muziki wa aina nyingine kama muziki wa dansi, watu wengi hata katika sherehe mbalimbali kwa mfano sherehe labda za harusi au kwa mfano hasa kwa wakristo kwa sababu nyimbo za injilini za wakristo, kwa hiyo katika sherehe nyingi za harusi au sherehe za komunio au ubarikio, wengi wanatumia muziki wa injili katika kuifanikisha ile sherehe. Na kuna waimbaji wengi ambao wameibuka hivi karibuni. Kuna waimbaji wazuri sana katika nyimbo hizi za injili. Kwa mfano kuna Jenifer Mgendi, kuna Rose Mhando, kuna waimbaji wengi sana, kuna Bahati Bukuku, na kuna wengine wengi ambao wameibuka katika huu muziki wa injili. Kwa hiyo utakuta nyimbo zao nyingi zinapigwa katika aah! hizi sherehe. Pia kuna kwaya mbalimbali, kwa mfano kama kwaya ya Kijitonyama nayo ina nyimbo nyingi sana ambazo huwa zinapigwa wakati wa sherehe. Na watu wengi wameupenda sana muziki wa injili kwa sasa kwa Tanzania kwa sababu licha ya muziki huo kueneza neno la Mungu, pia vilevile huu muziki unaelimisha pia jamii. Unaelimisha jamii katika aah! fani mbalimbali. Tofauti na muziki mwingine kwa mfano wa kizazi kipya,huu wa bongo flava, nyimbo nyingikatika muziki huu utakuta nyingi zinazungumzia suala zima la mapenzi, kitu ambacho na ni vijana ndio ambao unajua ndio kizazi kipya ni vijana ndio ambao wanapenda kusikiliza masuala hayo ya mapenzi lakini tunaona wengi hawapendi sana kusikiliza hizo kwa sababu aah! Wanasema kwamba inachangia sana kuhamasisha,labda watanzania katika suala zima la kufanya mapenzi na hivyo kuweza kufanya ukimwi, huu ugonjwa wa ukimwi uzidi kusambaa kwa sababu nyimbo nyingi zinazungumzia kuhusu suala zima la mapenzi

ambapo ndipo inahamsha hisia za kufanya mapenzi na wengi wanaishia kwenda kufanya mapenzi ambayo sio salama na baadae wanapata ukimwi. Kwa hiyo watanzania wengi wanapenda sana kusikiliza hizi nyimbo za muziki wa injili katika kipindi hiki cha miaka ya hivi karibuni kwa sababu licha ya kuelimisha jamii kuhusu neno la Mungu, lakini vilevile nyimbo zao nyingi zinaelimisha jamii.

**English translation:**

In Tanzania we have different types of music, like dance music and *bongo flava* for the new generation, because it is the younger generation who likes this kind of music. That's why we call it *bongo flava*. Bongo is the nickname for Dar es Salaam, which is the biggest city in the country. So they call it *bongo flava* because it originated in Dar es Salaam before spreading to other parts of the country. We also have traditional dance and gospel music. In recent years, gospel music has gained popularity in every part of the country. For celebrations such as weddings, Holy Communion, and child dedication, Christians, in particular, prefer gospel music over other types of music. There are really good gospel singers like Jennifer Mgendi, Rose Mhando, Bahati Bukuku and others whose songs are popular in the various celebrations I have mentioned above. Also there are gospel choirs like Kijitonyama in Dar es Salaam and other choirs which have good songs that people like. Many Tanzanians like to listen to gospel music because it not only educates people about the word of God, but it also educates the society on different issues. It is quite different from other types of music like *bongo flava* because most songs in *bongo flava* talk about love affairs. Those who prefer *bongo flava* are for the most part young. Because of that, many people, especially adults and Christians, don't want to listen to it because they say it is against their faith and it encourages people, especially young people, to have sex. By so doing, they spread the HIV/AIDS virus as a result of unsafe sex. So many Tanzanians prefer gospel music because it doesn't only educate them about the word of God, but it also teaches them about different issues.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated